# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA JOACHIM LEONARD WANGABO KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI YANAYOFANYIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA TAREHE 01/12/2017

***Ndugu Mwenyekiti wa CCM Mkoa,***

***Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,***

***Ndugu Makatibu Tawala wa Wilaya,***

***Ndugu Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa,***

***Ndugu Viongozi wa Madhehebu ya Dini,***

***Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,***

***Ndugu Viongozi wa Vyama vya Siasa,***

***Ndugu Viongozi wa Asasi za Kiraia,***

***Ndugu wageni waalikwa,***

***Mabibi na mabwana.***

Awali ya yote napenda kuupongeza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na wananchi wote wa Manispaa ya Sumbawanga kwa kukubali kuchukua jukumu la kuandaa maadhimisho haya ya siku ya UKIMWI Duniani Kimkoa. Pia napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa waratibu wa Mkoa wa Rukwa kwa kazi ya kutoa msaada na ushauri wa kitaalamu kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI Mkoani Rukwa. Pia napenda kuyapongeza mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kwa ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za mapambano dhidi ya UKIMWI likiwepo shirika la Waltereed kama mdau mkubwa Mkoani kwetu kwa kusaidia Asasi ndogondogo ili ziweze kuifikia jamii.

**Nduguwananchi,**

Kama mnavyofahamu, leo ni siku ya kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani. Tanzania ikiwa ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa inaungana na Mataifa mengine yote Ulimwenguni katika kuadhimisha siku hii muhimu. Maadhumuni ya maadhimisho haya ni kuikumbusha jamii Ulimwenguni pote kuendeleza

mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na kukabiliana na changamoto zote zinazoambatana nao.

**Ndugu Wananchi,**

Tatizo la UKIMWI linazidi kuongezeka na kumaliza nguvu kazi na kuziacha familia katika hali ya umaskini na majonzi makubwa. Kwa hiyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kujihoji juu ya hatua aliyochukua ili kukabiliana na janga hili hatari, sambamba na kuwasaidia watoto walio katika mazingira magumu baada ya wazazi wao kufariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, pia tunatoa mchango gani katika kuwasaidia wagonjwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwa kuwaona ni binadamu wenzetu wanaostahili kupata haki zote za kibinadamu kama binadamu wengine.

**Ndugu Wananchi,**

UKIMWI umekuwepo nchini kwa kipindi kisichopungua miaka 34, ni wazi kuwa ugonjwa huuu nafahamika na wengi wetu ikiwa ni pamoja

na jinsi unavyoambukizwa. (Takwimu zinaonyesha kuwepo kwa kiwango cha juu cha ufahamu kwa wananchi walio wengi Mkoani Rukwa). Ili kuthibitisha ukweli huu, matokeo ya utafiti wa UKIMWI na Malaria (THMIS) uliofanywa na ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2012, unaonyesha kuwa Zaidi ya asilimia 90 ya watu wazima wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 Mkoani Rukwa wanauelewa wa jinsi UKIMWI unavyo ambukizwa na jinsi ya kujikinga.

**Ndugu Wananchi,**

Pamoja na kuwepo kwa uelewa huo, bado hali ya maambukizi ya UKIMWI inazidi kutishia maisha ya watu hapa Mkoani kwetu. Kadri siku zinavyokwenda tunashuhudia vijana na watu wazima wakipoteza maisha na kuacha ongezeko kubwa la watoto yatima, wajane na wazee wasiokuwa na watu wa kuwatunza. Hali hii inatokana na kuendelea kupuuzwa kwa ushauri utolewao na wataalam juu ya namna ya kujikinga na UKIMWI. Matokeo yake watu wanaendelea kuwa na wapenzi wengi na kufanya ngono zisizo salama (yaani ngono zembe). Ukweli kuhusu

vitendo hivi unadhihirishwa na ushahidi wa matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2012 ambapo, wanaume 20 kati ya mia moja (100) walikuwa na wapenzi Zaidi ya wawili na wanaume ishirini na mbili (22) kati ya mia moja (100) walifanya mapenzi bila kutumia kinga ya mpira wa kiume yaani kondom.

**Ndugu Wananchi,**

Ujumbe wa mwaka huu unasema **CHANGIA MFUKO WA UDHAMINI WA UKIMWI: OKOA MAISHA, TANZANIA BILA UKIMWI INAWEZEKANA" Dhima kuu ya** Kaulimbiu hii ni kuhamasisha jamii katika uchangiaji wa mfuko wa udhamini wa Kudhibiti UKIMWI Nchini (AIDS Trust Fund-ATF). Mfuko huu ulianzishwa kupitia marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kuthibiti UKIMWI Na. 6 ya mwaka 2015. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni mkakati wa serikali kuwa na Mfuko wake na sio kutegemea wafadhili kwa asilimia mia moja.

**NduguWananchi,**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wadau kama mashirika yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Dini, imemejitahidi kueneza elimu kwa wananchi wa rika na jinsi zote walio maeneo ya mijini na vijijini namna ya kujikingana UKIMWI. Jitihada hizi zitazidi kuendelezwa ili kuona kuwa kila mara mwananchi anakumbushwa juu ya kujikinga dhidi ya maambukizi mapya. Napenda kutoa wito kwa wale wanaohusika na upangaji wa mipango katika Serikali na mashirika mengine ya umma na mashirika binafsi, kuhakikisha suala la elimu ya UKIMWI linapewa kipaumbele.

**NduguWananchi,**

Elimu ya kujikinga na UKIMWI haitoshi peke yake katika kukabiliana na ueneaji wa ugonjwa huu. Serikali wakati wote imekuwa ikihimiza juu ya kusubiri, kuwa na mpenzi mmoja au kuchukua tahadhari ya kufanya ngono salama wakati yote mawili yanashindikana. Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafanya ngono salama, serikali imekuwa ikitenga katika bajeti yake fedha kwa ajili ya kununua mipira ya kiume na ya kike kwa

ajili ya wanawake. Hata hivyo bado mwitikio sio mzuri kama mlivyosikia kwenye takwimu hapo awali bado kuna watu wengi ambao wanafanya ngono bila kinga.

**NduguWananchi,**

Suala la matibabu linapewa kipaumbele katika kukabiliana na ugonjwa huu. Baadhi ya mikakati ya kimatibabu katika kukabiliana na kueneakwa UKIMWI hapa Mkoani kwetu ni kuanzishwa kwa huduma ya kutibu magonjwa ya ngono, kufanya tohara kwa wanaume na pia kuzuia maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kutokana na mwitikio mzuri wa wananchi wanaojitokeza kwa wingi katika kupata tohara na akina mama kupata huduma ya kuzuia maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto.

**NduguWananchi,**

Risala imegusia masuala mbalimbali yanayosababisha maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI katika Mkoa na hususani katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Masuala hayo ni pamoja na ulevi uliokithiri, mila

na desturi za kurithi wajane na wagane, kuwa na wapenzi wengi na wanaofanya ngono zembe. Aidha takwimu zinaonyesha kuwa wanawake wameathirika Zaidi kuliko wanaume hii ni kutokana na mfumo dume ambao mwanamke hana maamuzi ya kufanya ngono.

**NduguWananchi**,

Mwisho naomba niwashukuru wananchi kwa kushiriki katika maandamano ambayo yamepamba maadhimisho haya. Jambo naloliacha kwenu ni kuwataka tushirikiane kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI bila kusahau kupiga vita Unyanyapaa na ubaguzi kwa WAVIU ili kuweza kufikia sifuri tatu na tisini tatu zilizoelezwa kwenye risala.

**“CHANGIA MFUKO WA UDHAMINI WA UDHIBITI WA UKIMWI NCHINI UOKOE MAISHA, TANZANIA BILA UKIMWI INAWEZEKANA”.**

***Asanteni kwa kunisikiliza.***